## Maswali

1. Mwanafunzi gani alikuwa muovu?
2. Alifanya nini?
3. Nini ilifanyika kwa Bustani ya Gethsemane?
4. Nani alisema kwamba lazima Yesu asulibiwe?
5. Wanawake walienda wapi siku ya kwanza ya juma?
6. Nini ilifanyika walipofika kwa kaburi?
7. Nini ilifanya ndiyo wanafunzi wakakubali kwamba Yesu alikuwa hai tena?
8. Yesu alipeleka wanafunzi wapi baada ya siku 40
9. Nini ilifanyika kwa Yesu kwa Mlima wa Mzeituni?
10. Yesu alienda wapi?
11. Malaika waliambia wanafunzi eti nini?

## Majibu

1. Yuda Iskariote alikuwa muovu.
2. Alikubali kusaidia wakuu wa makuhani kumkamata Yesu bora wampe pesa.
3. Yuda aliwaleta askari kwa Bustani ya Gethsemane. Alimbusu Yesu na Yesu akakamatwa. Wanafunzi walitoroka.
4. Pilato alisema lazima Yesu asulibiwe?
5. Wanawake walienda kwa kaburi kwenye Yesu alikuwa amezikwa.
6. Waliona jiwe limefiringishwa kando. Waliona malaika 2 waliowambia kwamba Yesu yu hai tena.
7. Yesu alikuja kwa nyumba walikokuwa. Walimgusa na kuzungumza naye.
8. Yesu alipeleka wanafunzi kwa Mlima wa Mzeituni.
9. Yesu alinyanyuliwa hewani na kupotelea ndani ya mawingu.
10. Yesu alienda kuishi na Mungu Mbinguni.
11. Malaika waliambia wanafunzi kwamba Yesu atakuja tena hapa duniani.

**SHULE YA JUMAPILI YA CBM**

**Awamu ya 1    Mwaka wa 3**

# 45 Yesu anakufa na anaishi tena

## Marejeo

Marko 14: 10 – 11; Luka 23: 44 – 46; 24: 1 – 10 na 36 – 43; Matendo ya Mitume 1: 9 – 11

## Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba alikubali kuawa kwa sababu alimpenda Mungu sana na alitaka kutupa sisi nafasi ya kuishi milele kwa Ufalme wa Mungu. Atarudi tena hapa duniani.

## Maneno maalum

45.1 Yesu + Yerusalemu + kufa + penda Mungu + tupee nafasi ya kuishi kwa Ufalme wa Mungu milele

45.2 Yuda Iskariote + wakuu wa makuhani + pesa + shika Yesu + Gethsemane + askari + busu +Yesu akamatwa

45.3 Yesu anahukumiwa + Kuhani Mkuu + Pilato + juu ya mlima +Sulibisha

45.4 Siku ya kwanza ya juma + wanawake + kaburi + jiwe limefiringishwa kando + malaika wawili + Yesu yu hai + ambia wanafunzi + Yesu + wanafunzi + alimguza na wakazungumza + Yesu yu hai

45.5 Siku 40 + Yesu + Mlima wa Mzeituni + Yesu alienda juu

45.6 Wanafunzi + malaika + Yesu atarudi tena

**45.1** Yesu alisafiri kwenda Yerusalemu. Mungu alikuwa ameambia Yesu kwamba atakufia kule. Yesu alimpenda Mungu na hakukuwa na shaka kwa sababu alijua Mungu atamfufua na awe hai tena. Yesu alijua kifo chake kitampa kila mtu nafasi ya kusamehewa dhambi zao na waishi milele kwa Ufalme wa Mungu hapa duniani.

**45.2** Mwanafunzi mmoja jina lake Yuda Iskariote, alikuwa muovu. Aliendа kwa wakuu wa makuhani na akawaahidi kuwasaidia kumshika Yesu ikiwa watampa pesa. Wakuu wa makuhani wakaahidi kumpa vipande thelathini vya fedha akiwasaidia kumkamata Yesu. Baadaye Yuda alijua kwamba Yesu alikuwa anaenda kuomba kwa Bustani ya Gethsemane. Akaenda kwa wakuu wa makuhani na akawambia kwamba watamshikia Yesu kule. Wakuu wa makuhani wakatuma askari kwenda kumkamata Yesu.

Yesu alipokuwa ako kwa Bustani ya Gethsemane na wanafunzi wake, aliona askari wakija na mapanga na marungu. Yuda aliwaongoza, alikuja mpaka kwa Yesu na akambusu kama ishara aliyokuwa amewapa wakuu wa makuhani. Yesu alikamatwa na kuchukuliwa. Wanafunzi waliogopa na wakatoroka.

**45.3** Yesu alihukumiwa kwa Kuhani Mkuu na siku iliyofuata alipelekwa kwa Pilato. Watu walisema uongo juu ya Yesu na wakasema kwamba anastahili kufa. Watu wote walipaza sauti wakisema anastahili kusulibiwa. Pilato aliajilia Yesu kwa askari na akawambia wamsulibishe.

Yesu alipelekwa inje ya Yerusalemu, juu ya mlima na kule alipigiliwa msalabani kwa misumari mpaka akafa. Mtu aitwaye Yusufu alimchukua na kumzika kwa kaburi mpya halafu wanafunzi wake wakaenda nyumbani wakiwa na huzuni.

**45.4** Siku ya kwanza ya juma baada ya kufa kwa Yesu, wanawake fulani walienda kaburini mwa Yesu kumpaka mafuta. Walipofika walishangaa kabisa kuona jiwe likiwa limefiringishwa kutoka kaburini. Malaika wawili walikuwa wamesima karibu na kaburi. Waliambia wale wanawake kwamba Mungu amemhuisha Yesu na yuko hai tena. Wale wanawake walifurahi sana na wakakimbia wawezavyo kwenda kuambia wanafunzi hiyo habari njema.

Wanafunzi walikuwa na huzuni sana sana kwa sababu Yesu alikuwa amekufa. Walifikiri hawatamuona tena. Wale wanawake walipofika na hiyo habari ya ajabu kwamba Yesu amefufuka na yu hai tena, wanafunzi hawakujua wafikirie nini – labda wale wanawake walikuwa wamefanya makosa.

Wanafunzi walikuwa kwa orofa wakizungumza. Walikuwa wanawaza kama wakubali kwamba Yesu amekuwa hai tena. Punde tu, Yesu mwenyewe aliwatokezea kule kwa kichumba walikokuwa. Walimgusa na wakazungumza naye. Hapo walikuwa na uhakika kwamba Mungu amefanya hiki kitendo cha ajabu – MUNGU AMEMFUFUA YESU KUWA HAI TENA.

**45.5** Baada ya siku arobaini, Yesu alijua kwamba ni wakati wake yeye kwenda kuishi na Mungu Mbinguni. Yesu aliwachukuwa wanafunzi wake, wakaenda kwa Mlima wa Mzeituni ulioko karibu na Yerusalemu. Yesu aliwambia kwamba atawasaidia kwa kazi yao.



Punde tu, alipokuwa bado anazungumza nao, Yesu alinyanyuliwa kutoka kwao. Yesu aliendelea kwenda juu na juu angani mpaka akapotelea ndani ya mawingu. Wanafunzi hawangeweza kumwona tena. Walibaki pale wakiangalia mawinguni penye alikuwa amepotelea.

**45.6** Halafu wanafunzi wakasikia mtu anazungumza nao. Waligeuka na wakaona malaika wawili wamesimama karibu nao.

Malaika waliambia wanafunzi kwamba siku moja Yesu atarudi hapa duniani kwa njia hiyo hiyo yenye wamemwona akienda. Yesu atakapokuja tena, atakuja kuwa Mfalme wa ulimwengu mzima. Atafanya ulimwengu kuwa mahali pa ajabu tena pa amani. Atawezesha kila mtu kuwa na furaha. Tunatumaini na kutarajia kwamba atakuja hivi karibuni.